

**SALAMU ZA WAAJIRI KUTOKA KWA BI. SUZANNE NDOMBA DORAN,
MKURUGENZI MTENDAJI WA ATE WAKATI WA KILELE CHA
MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA DUNIANI TAREHE 28
APRILI 2022 KATIKA VIWANJA VYA JKCC, DODOMA**

**Mgeni Rasmi, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb), Waziri OWM- Kazi, Ajira, Vijana
na Watu Wenye Ulemavu,**

**Mh. Patrobas Katambi (Mb) Naibu Waziri OWM- Kazi, Ajira, Vijana na Watu
Wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu,**

**Prof. Jamal Katundu, Katibu Mkuu, OWM- Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye
Ulemavu**

Waheshimiwa Viongozi wa Serikali mlioko hapa,

Waheshimiwa Wabunge mliopo,

Waheshimiwa viongozi kutoka Vyama vya Wafanyakazi,

Wadau wetu wa UTATU mlioko hapa,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa!

Nawasalimia kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru OSHA kwa mwaliko wa kuja kujumuika nanyi katika shughuli hii ya **Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Duniani** yenye lengo la kuhamasisha waajiri na wafanyakazi kuendelea kuzingatia Afya na Usalama Kazini. Pongezi za dhati ziwaendee Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kuandaa maadhimisho haya.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kinatambua umuhimu wa siku hii ambayo inatambulika Kimataifa kama Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ambapo Tanzania huungana na

mataifa mengine duniani kwa ajili ya kuiadhimisha siku hii na kauli mbiu ya Mwaka huu :
“Kwa pamoja tushirikiane kujenga utamaduni bora wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Act Together to build a Positive Safety And Health Culture)” ni sahihi katika kipindi hiki ambapo dunia inaendelea kupamabana na janga la UVIKO 19. Na sisi Chama cha Waajiri tumeendelea kuwasisitiza na kuwahamasisha Waajiri katika kuchukua tahadhari mahala pa kazi ili kupunguza madhara ya UVIKO., pamoja na kuwajengea uwezo waajiri katika maeneo ya Afya na Usalama mahali pa kazi. Mathalani matumizi sahihi ya vifaa vya kujikinga (Personal Protective Equipments) na pia athari za magonjwa yatokanayao na kazi za kukaa (Ergonomic hazards) na kutoa elimu pamoja na uhamasishaji kwa waajiri kuwaonyesha namna bora ya kutoa msaada kwa wafanyakazi wenye ulemavu.

Lakini pia nitumie fursa hii kuwasihii wafanyakazi kutumia vifaa kinga mahala pa kazi ili kuzuia magonjwa yatokanayo na kazi na ajali kazini.

Mheshimiwa Mgeni rasmi,

Tunaishukuru Serikali kwa jitihada kubwa katika kupunguza tozo za OSHA lakini pamoja na jitihada hizo, Chama cha Waajiri Tanzania tunaendelea kupendekeza kushushwa kwa gharama zinazotozwa mathalani tozo za upimaji wa afya za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mgeni rasmi,

Napenda nihitimishe salamu zangu kwa kuwapongeza Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) kwa maandalizi mazuri. Niwapongeze Washindi watakaoshinda leo na kuwahamasisha Waajiri wengine kujifunza bila kuchoka na kufuata Sheria ya afya na Usalama Mahala pa Kazi ili kuepuka migogoro lakini zaidi kulinda Afya za wafanyakazi mahala pa kazi lakini pia niwasihii Wafanyakazi kutumia vifaa kinga vinavyotolewa na Waajiri wao mahala pa kazi. Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) tunawaahidi kuendeleza ushirikiano wetu katika kutoa elimu kwa Waajiri ili kulinda Afya na Usalama mahala pa kazi.

Mwisho nawatakieni kila la kheri katika kuadhimisha siku hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza!